

**Theme: RESPONDING TO HIV/AIDS IN
SPECIAL GROUPS – REFUGEES
AT SECOND NATIONAL AIDS
CONFERENCE IN TANZANIA
ARUSHA – DECEMBER 16 – 20
DECEMBER, 2002**

**BY: RWEKAZA C.M
TITLE: SECRETARY GENERAL
FROM: ASEECA (NGO)
P.O. BOX 702 BUKOBA
Tel: 0744 – 760429
E-mail: aseccaspeed@hotmail.com**

Mkimbizi:

Mkimbizi ni mtu au raia aliyehama nchi yake kwa kulazimishwa au kutokana na kutishiwa usalama wa maisha yake na kwenda kuishi nchi ya ugenini.

Tanzania imekuwa na historia ya kupokea wakimbizi tangu miaka 60 hadi sasa 2002, na inaonekana itaendelea kupokea wengi kwa miaka ijayo kama hali ya kisiasa katika nchi za za maziwa makuu itaendelea kama ilivyo sasa.

Wamekuwepo wakimbizi kutoka Afrika Kusini, Msumbiji, Zimbabwe, Rwanda, Burundi, Uganda, Kenya DRC na hata nchi za mashariki ya Kati kama Palestina na sasa Iraq.

Sababu kuu ni kwamba katika nchi hizo kutokuwepo na utawala bora kwa raia wake. Wimbi kubwa la wakimbizi tutakalogusia ni kutoka katika maziwa makuu yaani Congo – DRC, Rwanda na Burundi, wanaoishi katika makambi kwenye mikoa ya Kagera, Kigoma, Rukwa, Magharibi mwa Tanzania.

Hakuna idadi sahihi ya wakimbizi waliopo kutokana na wakimbizi wengi kutoroka katika makambi kuishi uraiani, msituni na wengine kurudi katika nchi zao za awali inakadiriwa wapo kati ya 100,000 hadi 120,000.

HALI HALISI YA UKIMWI UNAVYOENEA KWA WAKIMBIZI:

Baada ya kuvuka mpaka na kusailiwa hupewa tunubari linalofanana na hema kwa kulitumia kama nyumba. Maisha mapya huanza kwa kutegemea misaada.

Kubakwa:

- Wanawake na wasichana wengi wao wanabakwa wakati wa kwenda kuchota maji au kutafuta kuni, hivyo huwa rahisi kuambukizwa virusi vya UKIMWI.

Faragha

- Wakati wa usiku baba na mama hulazimika kuhusiana kimwili na watoto wakiangalia , kusiikia vitendo hivyo hali inayosababisha vijana hao kuanza kujaribu mchezo huo mapema.

Elimu:

- Kwenye kambi hakuna elimu ya kutosha juu ya madhara yatokanayo na kufanya vitendo vya ngono isiyo salama kwa kutumia Kondomu na mpenzi mmoja.

Ufukara:

- Chakula (Posho) kinachotolewa makambini hakitoshi hivyo wakimbizi wa kike hulazimiika kutoa miili yao ili wapate mgao wa kutosha.
- Wakimbizi wa Afrika hupatiwa pungufu ya dola 1 wakati wa Ulaya ni zaidi ya dola 2 - mfano wakimbizi wa Bosinia.

KAMPENI YA KUTOA ASKARI WENGI KWA AJILI YA KUTAWALA BAADAYE:

- Pamekuwepo na kampeni ya kikabila kati aya WATUSI NA WAHUTU, (RWANDA NA BURUNDI) kwamba wanatakiwa wazaane sana ili hapo baadaye wawe na askari wengi ili wapindue serikali iliyopo madarakani. Hivyo akina mama wakishahamasika wako tayari kuzaa na mtu yejote bora apatiwe mtoto.

UZAZI WA MPANGO:

- Kwa utaratibu huu pia hawaelimishwi juu ya uzazi wa mpango.

KUHAMIA MIJINI:

- Wanawake walioathirika au ambao hawana mabwana hulazimika kutoroka makambini na kwenda katika miji au vijiji jirani huko huuza miili yao na kuendelea kueneza UKIMWI.

MAHITAJI YA MWILI

- Wanawake waliofiwa na waume zao wao kama binadamu wanahitaji kujamiihana hivyo hulazimika kutembea na mwanaume bila ya kumfahamu kama ameathirika au la.

UZURI WA ASILI KWA WANAWAKE WAKIMBIZI

- Wafanyakazi makambini/au wanaozunguka makambi jirani wanalazimika kuwatongoza wasichana au wanawake maana wamezaliwa na MVUTO WA ASILI usiokwepeka kwa mwanaume yejote hii inasaidia kueneza UKIMWI kwa haraka – NATURAL BEUTY..

MAPENDEKEZO – HITIMISHO

- Serikari zetu hasa za maziwa makuu ziwe za kuchagaliwa, kidemokrasia na zitende haki kwa raia wake.
- Wakimbizi wanaorudishwa kwao wahakikishiwe usalama wao na mali zao ili isiwe mchezo wa kundoika leo na kurudi kesho.
- Mandhari Tanzania imesaini mkataba wa Geneva – VOLUNTARY REPATRIATION FOR REFUGEES. Wakimbizi warejeshwe kwao kwa hiari yao na kuandaliwa mazingira mazuri kwao.
- Mataifa makubwa yaache kusambaza silaha ndogo ndogo, (SMALL ARMS) kwa nchi zetu changa. Hii itasaidia kupunguza wimbi la kutumia silaha kufanya unyanganyi, ubakaji hapa Tanzania na katika eneo la maziwa makuu.
- Mashirika ya kimataifa yasaidia nchi hizi kwa DHATI kuondoa umaskini.
- Mashirika hayo yaisaidie Tanzania kujenga miundombinu iliyoharibiwa na wakimbizi mfano mazingira, barabara n.k.

- Mashirika ya Hiari (NGO) ya nje yashirikiane au (SUB-CONTRACT) baadhi ya shughuli zao kwa NGO za Tanzania kwa baadhi ya shughuli zao katika kambi za wakimbizi zilizopo Tanzania.
- Uwepo usalama wa kutosha kambini ili kuzuia wanawake kunyanyaswa na KUBAKWA.
- Itolewe elimu juu ya maambukizi ya HIV/AID na UZAZI WA MPANGO.
- Serikari za maziwa makuu zishirikishe wadau wote katika kutatua matatizo ya nchi zao ili yamalizike ili tusizalishe wakimbizi tena utaratibu wa sasa umeonyesha kushindwa kwa kuwashirikisha kwa wanajeshi na wanasiaya. K.m. vikundi vya wanawake, NGO, wafanyabiashara.

UKIMWI HAUBAGUI SISI TUNABAGUA

TUSAIDIE KUONDOA TATIZO SHUKRANI